Mafunzo ya wasaidizi Ustawi wa Jamii awamu ya pili :

Stadi za kushughulikia watoto waishio katika mazingira hatarishi zaidi na familia katika mazingira maalumu.

Siku ya 4

Ulinzi wa mtoto, unyanyasaji wa mtoto, na upimaji wa hatari na uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira

Malengo

kufikia mwisho wa mada hii kila mshiriki aweze ku:

- Eleza maana ya unyanyasaji wa mtoto na kutojaliwa kwa Tanzania.
- Elezea madhara ya unyanyasaji kwa mtoto
- Tambua sababu zinazofanya mtoto, mzazi, na mazingira yao yanayomuweka mtoto katika hatari ya unyanyasaji na kutojaliwa
- Tambua sababu zinazoweza kusaidia ulinzi wa watoto dhidi ya unyanyasaji na kuendeleza uwezo wa mtoto, familia kukabiliana na hali kulingana na mazingira.
- Tengeneza shughuli zitakazo punguza hatari na endeleza sababu za ulinzi na zitakazo muwezesha mtoto na familia kukabiliana na hali kulingana na mazingira.

Nini Maana Ya Unyanyasaji Wa Mtoto?

Bangua Bongo

Unyanyasaji Wa Mtoto Na Haki Za Mtoto Nchini Tanzania

- Unyanyasaji wa mtoto una maana ya uvunjaji wa sheria kuhusu haki za mtoto kunakopelekea athari za kimwili, kimaadili au kihisia ikiwemo vipigo, kutukanwa matusi, kubaguliwa, kutojaliwa unyanyasaji wa kingono na utumikishwaji.
- Haki za mtoto zimelengwa moja kwa moja katika sheria ya mtoto nchini Tanzania ya mwaka 2009 kama ifuatavyo :

Haki Za Mtoto

- ***Mtoto chini ya miaka 18 atakuwa na haki ya:***
  - Kuishi huru dhidi ya ubaguzi wa aina yeyote
  - Kuwa na jina, utaifa au kufahamu wazazi wake wa asili na ndugu wengine wa familia.
  - Kuishi na wazazi wake au walezi.
  - Isipokuwa tu kama kuishi na wazazi au familia
  - kutapelekea madhara kwa mtoto, kutamuweka mtoto katika hatari ya unyanyasaji wa hatari au
  - -Hakutna manufaa bora kwa mtoto.

Haki Za Mtoto Zinaendelea…

Kwa :
- Chakula
- makazi
- mavazi
- Huduma za afya ikiwemo Huduma za chanjo immunizations
- Elimu na muongozo
- Uhuru
- Haki ya kucheza

Toka kwa wazazi wake:
- Kuishi
- Utu
- Heshima
- Starehe
- Uhuru
- Afya
- Elimu
- Makazi

Wajibu Wa Wazazi:

- ***Kumlinda mtoto dhidi ya:***
  - kutojaliwa
  - Kumbagua na ukandamizaji
  - Vurugu
  - Unyanyasaji
  - Mazingira ya hatari kimwili, kimaadili na yenye kukandamiza

Wazazi Wana Wajibu Wa:

- Kutoa malezi yenye muongozo mzuri, muendelezo wa msaada kwa mtoto kuhakikisha uhai wa mtoto na maendeleo.
- Uwe na uhakika kuwa kukosekana kwa muda kwa mzazi, mtoto atakuwa chini ya uangalizi wa mtu mwenye uwezo.

Haki Za Mtoto Za Ziada Nchini Tanzania.

- ***Urithi:*** Kufurahia miliki ya wazazi wake
- Kutoa mawazo yake. Mtu yeyote hapaswi kumnyima mtoto mwenye uwezo wa kutoa maoni haki ya kutoa maoni, kusikilizwa na kushiriki katika kufanya maamuzi yanayoathiri usalama wake.
- Epuka shughuli zenye madhara. Mtu hapaswi ku muajiri au kumhusisha mtoto katika shughuli yeyote inayoweza kuwa na madhara kwa afya ya mtoto, elimu, akili, mwili au maendeleo ya kimaadili.

Haki Za Mtoto Za Ziada Nchini Tanzania.

- Huru dhidi ya mateso au adhabu zisizo za kawaida ikiwemo vitendo vyenye dhamira ya kudhalilisha au kushusha utu wa mtoto.
- Huru dhidi ya mila zinazodhalilisha utu au zenye madhara kimwili, kiakili na kwa usalama wa mtoto.

Adhabu ya ukiukwaji wa haki hizi:

- Mtu yeyote atakaye hukumiwa kwa kosa la ukiukwaji
- wa sehemu ya sheria atawajibika kulipa faini isiyozidi
- shilingi laki tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi
- miezi sita au vyote viwili.

Muhtasari Kwa Ufupi: Haki Za Mtoto

Washiriki kutoa muhtasari ya mambo ya muhimu kuhusu haki za mtoto.

Majukumu Ya Mtoto Wa Tanzania

- ***Mtoto atakuwa na jukumu pamoja na wajibu wa:***
  - Kufanyakazi kwa ajili ya umoja wa familia
  - Kuheshimu wazazi wake, walezi, waangalizi na wakubwa wakati wote na kuwasaidia wanapokuwa na uhitaji
  - Kuitumikia Jamii yake na Taifa katika kutumia uwezo wake wa kimwili na kiakili katika huduma zake kulingana na umri na uwezo alionao.
  - Kuhifadhi na kuimarisha umoja wa kijamii na Taifa: na
  - Kuhifadhi na kuimarisha mila na desturi nzuri za jamii yake na Taifa kwa ujumla kwa kushirikiana na wanajamii wengine au Taifa

Maana ya mtoto anaehitaji ulinzi kwenye sheria ya mtoto ya mwaka 2009

16(1) Kwa kusudi la kifungu hiki , mtoto anahitaji huduma na ulinzi ikiwa mtoto huyo

a) Ni yatima au ametelekezwa na jamaa zake
b) Hajaliwi au amefanyiwa vibaya na mtu anayemhudumia au aliye chini ya uangalizi wake au mlezi au wazazi;
c) Ana mzazi au mlezi ambaye hana malezi mazuri
d) Anakosa mahitaji ya msingi kama chakula, mavazi, malazi,n.k.

Maana Ya Mtoto Anayehitaji Ulinzi Kwenye Sheria Ya Mtoto Ya Mwaka 2009

e) Yuko chini ya uangalizi wa mzazi au mlezi ambaye kwa sababu ya uhalifu au tabia za ulevi, hafai kuwa mwangalizi wa mtoto.
f) Anazururа na hana mahali anapoweza kuita nyumbani au makazi ya kuishi;
g) Anaomba au kupokea misaada kuwe ama kusiwe na kujifanya kuimba, kucheza, kufanya maigizo, kutoa kitu chochote ili kiuzwe au vinginevyo, au anakutwa mtaani, katikaa mazingira au mahali kwa lengo la kuomba au kupokea msaada.
h) Anaambatana na mtu yeyote wakati mtu huyo anapoomba au kupokea msaada, kuwe au kusiwe na kujifanya kuimba, kucheza, kufamnya maigizo, kutoa chochote ili kiuzwe au vinginevyo.

Inaendelea...

i) Yuko chini ya uangalizi wa mzazi anayekosa mahitaji muhimu kama vile chakula, mavazi, makazi.
j) Anaeambatana na mhalifu au kahaba;
k) Anaishi katika nyumba au sehemu ya nyumba inayotumiwa na kahaba kwa makusudi ya ukahaba au vinginevyo anaishi katika mazingira yanayokadiriwa kusababisha, kuwezesha au kuchangia ushawishi au ukahaba wa, au unaathiri maadili ya mtoto.
l) Je mtu huyo ana uhusiano na mtu aliyetendewa uhalifu au jaribio chini ya kifungu kinachokataza usafirishaji wa binadamu

Inaendelea...

m) Amekutwa akionyesha tabia ambazo zinaashiria kumshuku kuwa ana au amekuwa akishawishi au akilazimisha kwa lengo la uvunjaji wa maadili.
n) Yuko chini ya umri wa kuwajibishwa kisheria na anahusika katika kutenda uhalifu mbali na kosa dogo la shauri la kihalifu.
o) Kwa namna moja au nyingine yuko katika hatari ya kimaadili au kimwili
p) Yuko chini ya uangalizi wa mtu mwenye ulemavu na ulemavu huo una mzuia mtu huyo kuweza kumhudumia vizuri au uangalizi mzuri au
q) Katika mazingira mengineyo yeyote kama kamishna wa ustawi atakavyobaini

Maneno yanayoashiria unyanyasaji wa mtoto katika sheria ya mtoto 2009?

- Sheria ya mtoto ya Tanzania ina maneno kadhaa yanayoashiria kuwa mtoto ananyanyaswa
- Hii inahusisha “Unyanyasaji wa hatari” “kutendewa vibaya” “mateso, au ukatili mwingine, adhabu zisizo za ki utu au kufanyiwa udhalilishaji”

Kutambua unyanyasaji wa mtoto au kutojaliwa

Nini maana ya…

- Unyanyasaji
- Kutojaliwa
- Kutelekezwa

Nini maana…

- ***Unyanyasaji****:* Kudhuru mwili, Hisia/madhara ya kisaikolojia au vitendo vya kujamiiana na mtoto.
- ***Kutojaliwa****:* Uangalizi mdogo, usimamizi au msaada kwa mtoto
- ***Kutelekezwa:*** mtoto ambaye mzazi amemwacha moja kwa moja au kwa muda mrefu pasipo kufanya taratibu zingine kwa ajili ya uangalizi wa mtoto
- Utumikishwaji: kulazimishwa kufanya kazi au kutumia watoto kwa masuala ya ngono.

Je Ni Dalili Zipi Zinazoashiria Kuwa Mtoto Ana Nyanyaswa?

- Ni zipi dalili za awali unazoweza kuziona kwa mtoto au mzazi tabia ambazo zinaashiria hatari kuwa kuna uwezekano mtoto ananyanyaswa au kutojaliwa na uzizingatie?

Bangua Bongo

Dalili Za Unyanyaswaji Wa Mtoto Au Kutojaliwa.

- Dalili zifuatazo zinaweza kuashiria kuwa kuna unyanyasaji au kutojaliwa kwa mtoto. Ikiwa utazion chunguza uwezekano kuwa mtoto ananyanyaswa au kutojaliwa.

Mtoto:

- Anaonyesha mabadiliko ya ghafla ya kitabia au maendeleo ya shule
- Mtoto hajapatiwa msaada wa kimwili au matatizo ya kiafya yaliyoelezwa bayana kwa wazazi
- Ana matatizo ya kujifunza (ni vigumu kuwa makini) ambapo haiwezekani kuhusishwa mahususi na sababu za kimwili au kisaikolojia

Inaendelea...

- Mara zote anakuwa makini kama vile anajiandaa kwa kitu kibaya kutokea
- Anakosa uangalizi wa mtu mzima
- Anahusika sana na kufuata amri zaidi
- Anaepuka kutoa majibu(huwa mtulivu), au kama hayupo
- Hufika shuleni au kwenye shughulizinginezo mapema, hukaa mpaka muda umepitiliza sana na hataki kurudi nyumbani’

Kutambua Unyanyasaji Wa Mtoto Au Kutojaliwa

Mzazi:

- Anonyesha kuhusika kidogo sana na maswala ya mtoto
- Hukana kuwepo kwa au humlaumu mtoto kwa matatizo ya mtoto shuleni au nyumbani
- Huwaomba waalimu au walezi wengine kutumia ukatili au adhabu kali za kimwili ili kumuadibisha mtoto iwapo atafanya kosa
- Kumuona mtoto kuwa mbaya sana, asiye na thamani na ni mzigo
- Hutaka viwango vya kimwili au kitaaluma ambavyo mtoto hana uwezo wa kuvifikia
- Kimsingi humtegemea mtoto kwa huduma, kujaliwa na utoshelevu wa mahitaji ya kihisia

Kutambua unyanyasaji wa mtoto au kutojaliwa

Mzazi na Mtoto:

- Mara chache sana humgusa au hutazamana na mtoto
- Mara zote huona kuwa mahusiano yao ni mabaya
- Husema kuwa hawapendani

Dalili Na Aina Za Unyanyasaji/Kutojaliwa

- Dalili za unyanyasaji
  - Unyanyasaji wa kimwili
  - Kutojaliwa
  - Uyanyasaji wa kingono
  - Unyanyasaji wa kihisia
- Mara nyingi hutokea katika mchanganyiko wa zaidi ya dalili moja kuliko dalili moja peke yake
  - Mtoto aliyenyanyaswa kimwili, kwa mfano mara nyingi anayanyasika kihisia na mtoto aliye nyanyaswa kingono pia anaweza kutojaliwa

Zoezi: Kutambua Dalili Za Unyanyasaji Wa Mtoto Au Kubaguliwa

- Mjigawe katika makundi manne,
- Kila kundi lishughulikie aina mojawapo ya unyanyasaji likizingatia:
- Unyanyaswaji wa kimwili
- Unyanyaswaji wa kingono
- Kutojaliwa
- Unyanyaswaji wa kihisia
- wana vikundi wajibu maswali yafuatayo kutegemeana na aina ya unyanyasaji wanaoushughulikia:
- Ni dalili zipi zinazoashiria kuwa mtoto unayemshughulikia ananyanyaswa? Taja dalili nyingi za aina ya unyanyasaji unaoshughulikia
- Tumia dakika 10 kukamilisha kazi
- Muwe tayari kutoa mrejesho katika kundi kubwa.

Dalili Za Unyanyasaji Wa Kimwili

Fikiria kuwa kuna uwezekano wa unyanyasaji Kimwili

kwa mtoto ikiwa:

- Anavidonda visivyoelezeka vya moto, alama za kung’atwa, michubuko, mivunjiko ya mifupa na macho meusi
- Ana michubuko iliyofifia au alama nyinginezo zinazoonekana baada ya kutohudhuria shule.
- Huonyesha kuwaogopa wazazi na kupinga au hulia wakati wa muda wa kurudi nyumbani
- Husinyaa anapokutana na watu wazima
- Hutoa taarifa za kujeruhiwa na mzazi au mtu mzima mlezi

Dalili Za Unyanyasaji Wa Kimwili

Fikiria kuwa kuna uwezekano wa unyanyasaji Kimwili

kwa mtoto ikiwa:mzazi au mtu mzima mwingine Mlezi:

- Hutoa mawazo yenye mgongano, yasiyoshawishi na yasiyo na maelezo yanayoelezea sababu za majeraha ya mtoto
- Humwelezea mtoto kuwa “muovu”, au kwa njia nyinginezo zilizo hasi
- Hutumia adhabu za kikatili kwamwili wa mtoto
- Ana historia ya kufanyiwa unyanysaji akiwa mtoto

Unyanyasaji Wa Kingono

Fikiria kuwa kuna uwezekano wa unyanyasaji

Kimwili kwa mtoto ikiwa:

- Anatembea au kukaa kwa shida
- Ghafla anakataa kubadili kwa ajili ya mazoezi au kushiriki katika mazoezi ya mwili
- Anatoa taarifa za kupata ndoto au kukojoa kitandani
- Kubadilika ghafla kwa hamu ya kula

Dalili za Unyanyasaji Wa Kingono...

- Huonyesha tabia zisizo za kawaida, mambo nyeti sana au ufahamu usio wa kawaida kuhusu masuala ya kujamiiana au tabia
- Kuwa mjamzito au kupata magonjwa ya ngono hususan kama ana umri chini ya miaka 14
- Hukimbilia /hutorokea mbali
- Taarifa za kunyanyaswa kijinsia hutolewa na mzazi au mtu mzima mwingine anayemlea

Dalili Za Unyanyasaji Wa Kingono...

Ufikirie kuwa kuna uwezekano wa unyanyasaji wa kingono ikiwa mzazi au mlezi mwengine ambaye ni mtu mzima.

- Anamlinda mtoto isivyokawaida au anamdhibiti sana mtoto kutochangamana na watoto wenzie, haswa wa jinsi tofauti.
- Ni msiri sana na anajitenga
- Ni mwenye wivu au anayetawala wanafamilia wengine.

Dalili Za Kutojaliwa

Fikiria kuwa kuna uwezekano mtoto hajaliwi ikiwa:

- Hukosa vifaa/mahitaji muhimu vya shule
- Mara nyingi hukosa kuhudhuria masomo shuleni
- Huomba au huiba chakula au pesa
- Hukosa huduma za kitabibu anazohitaji au huduma za meno, chanjo au huduma za macho (miwani)
- Hukosa huduma za afya anazohitaji au chanjo.

Dalili Za Kutojaliwa...

Fikiria kuwa kuna uwezekano mtoto hajaliwi kiwa:

- Mara nyingi ni mchafu na anatoa harufu mbaya
- Hukosa nguo za kutosheleza kulingana na hali ya hewa
- Ni mlevi wa pombe au dawa za kulevya
- Hueleza kuwa hakuna mtu wa kumlea nyumbani

Inaendelea...

Fikiriai kuwa kuna uwezekano wa kutojaliwa mtoto ikiwa Mzazi au mtu mzima mwingine mlezi:

- Huonyesha kuwa kinyume na mtoto
- Huonyesha kuhuzunika au kuwa na sonona
- Huonyesha tabia zisizo na uwiano au tabia za ajabu ajabu
- Ni mlevi wa pombe kupindukia au anatumia dawa za kulevya

Dalili Za Kunyanyaswa Kihisia

Kunyanyaswa Kihisia inamaana ya kuwa mtoto anatendewa vibaya au anafanyiwa isivyo sawa:
Fikiria kuwa kuna uwezekano wa kunyanyaswa mtoto kihisia ikiwa:

- Anaonyesha tabia zisizo za kawaida - kama vile kusubiri kuamrishwa (Mlalamishi) au mtoto ana madai kupita kiasi, mkimya sana/mnyonge au yupo yupo tu, anakwepa shughuli, au mtoto anakuwa mkatili.
- Anakuwa na tabia au za kiutu uzima sana au za kitoto. Mtoto anakuwa na tabia ya mtu mzima isiyoendana na umri wake(Mfano, Kuwalea watoto wengine) au tabia isiyo ya kawaida kwa mtoto (Mfano, anajizungusha mara kwa mara au ana gonga gonga kichwa)

Dalili Za Unyanyaswaji Wa Kihisia…

- Ana kawia katika ukuaji wa kimwili na kihisia
- Ameshajaribu kujiua
- Hutoa taarifa za kukosa ukaribu na mzazi.

Dalili Za Uyanyaswaji Wa Kihisia…

Fikiria kuwa kuna uwezekano wa kunyanyaswa mtoto kihisia ikiwa mzazi au mtu mzima mwingine mlezi :

- Mara zote hulaumu, hujishusha, au humshusha kiwango mtoto
- Hajihusishi chochote na mtoto na hukataa msaada wowote wa kusaidia matatizo ya mtoto
- Huonyesha kumkataa mtoto

Jinsi Gani Unyanyasaji Unavyomuathiri Mtoto

- Ni pamoja na athari zote za wakati huohuo na athari za unyanyasaji za muda mrefu.

Madhara Ya Unyanyasaji Wa Mtoto

- Kwanini ni muhimu kujifunza kuhusu unyanyasaji wa mtoto/ kutojaliwa?
- Je unaamini nini kinaweza kuwa madhara ya unyanyasaji wa mtoto?

Bungua bongo/ Majadiliano

Jinsi Gani Unyanyasaji Au Kutojaliwa Kunavyo Muathiri Mtoto

- Matokeo ya unyanyasaji au kutojaliwa mtoto mara nyingi hujadiliwa kwa upande wa madhara. Madhara ni kile kinachotokea kama matokeo ya unyanyaswaji/ kutojaliwa. Hii huweza kuwa athari za:
  - Kimwili
  - Kisaikolojia
  - Kitabia
  - Kijamii

Madhara Ya Unyanyasaji Wa Mtoto/Kutojaliwa

- Mara nyingi madhara hutokea kwa wakati mmoja katika maeneo haya tofauti. Kusema kweli ni vigumu kuyatenganisha kabisa.
  - Athari za kimwili, kama kuathirika kwa ukuaji wa ubongo wa mtoto, yaweza kuwa na madhara ya kisaikolojia kama vile kuwa na ufahamu wa taratibu au matatizo ya kihisia
  - Matatizo ya kisaikolojia mara nyingi hujitokeza kama tabia hatarishi, sonona, na shauku, kwa mfano, inaweza kumfanya mtu kuwa mvuta sigara, mlevi wa pombe au dawa za kulevya au kula sana
  - Tabia hatarishi,matokeo yake huweza kupelekea madhara ya muda mrefu ya kimwili, matatizo ya kiafya, kama magonjwa ya ngono, saratani au kuwa na uzito mkubwa kuliko kawaida.

Athari Za Afya Ya Mwili

- Madhara ya haraka zaidi yatokanayo na unyanyasaji wa kimwili au kutojaliwa yanaweza kuwa madogo kama vile (michubuko au kukatwakatwa) au madhara makubwa kama (kuvunjika kwa mifupa, kutokwa na damu au hata kifo).
- Mara nyingine madhara ya kimwili huwa ni ya muda mfupi hata hivyo maumivu
- Anayopata mtoto na mateso huweza kuwa ya muhimu sana.
- Madhara ya muda mrefu ya afya ya mwili yatokanayo na unyanyasaji au kutengwa kwa mtoto ndio kwanza yanaanza kufanyiwa kazi ili yaweze kutambulika

Athari Za Afya Ya Mwili...

- Kulingana na utafiti wa Kitaifa wa Marekani kuhusu hali bora za watoto na vijana balehe (NSCAW), zaidi ya robo ya watoto waliokuwa katika malezi ya kambo kwa zaidi ya miezi 12 walikuwa na matatizo ya afya yanayodumu kwa muda mrefu au yanayojirudia rudia.
- ***Mtoto mwenye dalili za kutikiswa:***

  Utikiswaji wa watoto ni aina mojawapo ya unyanyasaji wa watoto madhara yatokanayo na kutikiswa yanaweza yasigundulike kwa haraka na yanaweza yakawa kuvuja kwa damu kwenye jicho au ubongo, athari katika uti wa mgongo au shingo, mivunjiko ya mbavu au mifupa (Kituo cha Taifa cha matatizo ya mfumo wa fahamu na kiharusi, 2007
- (Utawala kwa watoto na familia, ofisi ya mipango, utafiti na upimaji [ACF/OPRE], 2004a) Matokeo mengine ya tafiti ni kama ifuatavyo:

Athari Za Afya Ya Mwili…

- ***Matatizo ya ukuwaji wa ubongo:*** unyanyasaji wa mtoto na kutojaliwa mara nyingine husababisha kuto kuwa kabisa au kutokuwa vizuri kwa sehemu za ubongo kunakopelekea kushindwa kukua . Hali hii ina madhara ya muda mrefu kwa ufahamu, lugha na uwezo wa kitaaluma
- ***Afya duni ya mwili:*** Tafiti nyingi zimeonyesha uhusiano wa aina mbalimbali wa kushindwa kufanya kazi vizuri nyumbani (ikiwemo unynyaswaji wa watoto) na afya duni (Flaherty et al, 2006; Felitti, 2002). Watu wazima walio wahi kunyanyaswa au kutojaliwa utotoni wako katika hatari zaidi ya kupata madhara ya kimwili kama vile mzio(allrgy) Magonjwa ya viungo, pumu, homa ya mapafu, shinikizo la damu na vidonda vya tumbo. (Springer, Sheridan, Kuo, & Carnes, 2007)

Sources: 1. De Bellis & Thomas, 2003. 2. Watts-English, Fortson, Gibler, Hooper, & De Bellis, 2006. 3. ACF/OPRE, 2004a. 4. Flaherty et al., 2006; Felitti, 2002. 5. [5](Springer, Sheridan, Kuo, & Carnes, 2007).
Child Welfare Information Gateway. (2008). Long-term consequences of child abuse and neglect. Washington, DC: USDHHS

Athari Za Kisaikolojia

- Madhara ya haraka ya kihisia yatokanayo na kunyanyaswa na kutojaliwa –kutengwa, hofu na kukosa uwezo wa kumwamini mtu- yaweza kutafsiriwa katika madhara ya muda mrefu ikiwemo kutojiamini, sonona na matatizo ya mahusiano. Watafiti wamegundua uhusiano kati ya unyanyasaji na kutojaliwa na yafuatayo
- ***Matatizo wakati wa utoto:***
  Sonona na kujikataa ni kati ya dalili(withdrawal) zinazojitokeza sana kati ya watoto wa miaka mi 3 waliopitia kutojaliwa1 kihisia, kimwili, au kimazingira

Chanzo:1 springer, sheridan, kuo,& carnes, 2007.

Athari Za Kisaikolojia...

- ***Afya duni ya akili na kihisia:***
  Katika utafiti wa muda mrefu takriban 80 asilimia ya vijana waliowahi kunyanyaswa walifikia vigezo vya kutambulika kuwa na angalau tatizo mojawapo la Afya ya akili katika umri wa miaka 21.
  Vijana hawa walikabiliwa na matatizo mengi, yakiwemo sonona, kuwa na shauku, matatizo ya ulaji chakula, na kujaribu kujiua
  Matatizo mengine ya kisaikolojia na hali za kihisia zinazohusiana na kunyanyaswa na kutojaliwa ni pamoja na kuwa na wasiwasi, matatizo ya kutochangamana na wengine, Upungufu wa umakini/ Kuchangamka kupita kiasi, sonona, Hasira, Msongo wa baada ya mstuko wa maono, na matatizo ya kutoweza kuwa na ukaribu.

chanzo: 1, Silverman, Reinhertz, & Glaconia, 1996(Teicher, 2000; De Billis & Thomas, 2003; Springer, Sheridan, Kuo, 7 Crnes, 2007
(Silverman, Reinhertz, & Glaconia, 1996).

Athari Za Kisaikolojia…

- ***Matatizo ya Ufahamu:*** watoto walioletwa katika uangalizi ndani ya vituo kwa sababu za kunyanyaswa au kutojaliwa walikuwa na uwezo mdogo kiufahamu ukilinganisha na watu wengine katika vigezo vya kiufahamu, maendeleo ya lugha, na uwezo wa kitaaluma.
  Utafiti wa mwaka 1999 wa LONGSCAN pia uligundua uhusiano kati ya unyanyasaji uliowazi wa mtoto na maendeleo duni ya kitaaluma ikiwemo utendaji darasani kwa watoto walio katika umri wa kwenda shule
- ***Matatizo ya kijamii:*** Watoto waliowahi kukataliwa au kutojaliwa wako katika hatari zaidi ya kuwa na tabia za kutochangamana na wengine kijamii wanapokuwa watu wazima. Kutojaliwa na wazazi pia kuna uhusiano na kuwa na hali ya kukereka na tabia ya ugomvi

Chanzo: 1(Idara ya Afya na Huduma za watu ya Marekani , 2003). 2.Zolotor, Kotch, Dufort, Winsor, & Catellier, 1999) 3.Schore, 2003)

Athari Za Kitabia

- Si wahanga wote wa unyanyasaji wa watoto au kutojaliwa watapata athari za kitabia.
- Matatizo ya kitabia hutokea zaidi kati ya kundi hili hata katika umri mdogo.
- Utafiti uliofanywa kwa watoto wa umri wa miaka 3 hadi 5 walio katika malezi ya kambo waligundua kuwa watoto hao walikuwa na kiwango cha wastani cha matatizo ya kitabia kwa wastani zaidi ya mara mbili ukilinganisha na watu wengine.

Athari Za Kitabia...

- Hapo baadae katika maisha unyanyasaji watoto na kutojaliwa hupelekea uwezekako zaidi wa yafuatayo:
- ***Matatizo wakati wa ujana Balehe:*** Tafiti zimeonyesha kuwa karibu 25 asilimia ya watoto walionyanyaswa au kutojaliwa wana uwezekano wa kuwa na matatizo ya tabia mbaya, mimba za ujanani, maendeleo ya chini kitaaluma, utumiaji wa madawa ya kulevya na matatizo ya afya ya akili
- Tafiti nyingine zilipendekeza kuwa watoto1 walionyanyaswa au kutojaliwa walo katika hatari zaidi ya kujiingiza katika ngono hatarishi wanapofikia ujanabalehe, hivyo huongeza uwezekano wa kupata maambukizi ya magonjwa ya ngono2
- ***Tabia mbaya utotoni na uhalifu ukubwani:*** Kulingana na utafiti uliofanywa na kituo cha kisheria cha kitaifa, Watoto walionyanyaswa au kutojaliwa walikuwa na uwezekano wa mara 11 zaidi wa kukamatwa kwa tuhuma za matukio ya kiuhalifu wakiwa watoto, mara 2,7 zaidi uwezekano wa kukamatwa kwa sababu ya kufanya vurugu na tabia za kihalifu wakiwa watu wazima na mara 3.1 zaidi uwezekano wa kutiwa nguvuni kwa ajili ya moja ya aina ya uhalifu (utotoni au ukubwani) 3

Athari Za Kitabia...

- ***Unywaji pombe na utumiaji madawa ya kulevya:****Tafiti* mara zote zimekuwa zikionyesha kuongezeka kwa uwezekano wa matumizi ya pombe, uvutaji sigara na madawa ya kulevya katika maisha ya watoto walionyanyaswa au kutengwa Kulingana na ripoti ya kitengo cha Taifa cha kudhibiti Madawa ya kulevya, karibu theluthi mbili ya tatu ya watu walio katika programu ya tiba ya watumiaji madawa walitoa taarifa za kunyanyaswa wakati wa utoto.
- ***Tabia ya matusi:***Wazazi wenye tabia za matusi mara nyingi walifanyiwa unyanyasaji wakati wakiwa watoto. Inakadiriwa kuwa karibu moja ya tatu ya watoto walionyanyaswa au kutojaliwa hatimae na wao pia wata watendea vivyo hivyo watoto wao wenyewe

Chanzo: 1.(Kelly, Thomberry, & Smith 1997, 2. (Johnson, Rew & Sternglanz, 2006) (ACF, 2004b), 3. English, Widom, & Brandford, 2004) . 4.(Dube et al, 2001). 5. (Swan, 1998) 6. (prevent child Abuse New York, 2003).

Athari Za Kijamii

- Wakati unyanyasaji na kutojaliwa watoto karibu mara zote hutokea ndani ya familia, madhara yake hayaishii hapo tu. Jamii vilevile hulipa gharama kwa ajili ya unyanyaswaji na kutojaliwa kwa watoto kwa misingi ya gharama za moja kwa moja au gharama zisizo za moja kwa moja.
- ***Gharama za moja kwa moja:***Gharama za moja kwa moja zinajumuisha gharama za huduma za uchunguzi na kushughulikia malalamiko kuhusu unyanyasaji na kutojaliwa kwa mtoto
- Gharama za mfumo wa sheria, ikiwemo huduma za kimahakama, polisi na huduma za kijamii kushughulikia masuala ya unyanyasaji wa mtoto.

Athari Za Kijamii

- Kupotea kwa raia wenye thamani wanaoweza kuchangia katika jamii
- Gharama za kushughulikia matatizo ya mtoto hadi utu uzima. Hii ni pamoja na gharama zinazohusiana na uhalifu wa watoto na wa watu wazima , matatizo ya afya ya akili, utumiaji wa vilevi, na vurugu za majumbani. Kuongezeka kwa gharama za huduma za afya.
- Kupotea kwa uzalishajimali kwa kukosa ajira na kuajiri watu wachache

Mambo Yanayochangia Matokeo Ya Athari

- Je hali ya unyanyasaji wa mtoto huwaathiri watoto wote kwa namna iliyo sawa?
- Ikiwa sivyo, unafikiri ni sababu gani zinazofanya kuwe na tofauti?

Majadiliano

Tofauti Katika Mwitikio Wa Watoto Kuhusu Unyanyasaji

- Madhara yanaweza kuwa madogo au mabaya; yanayoweza kupotea baada ya muda mfupi au yanayoweza kudumu kwa maisha yote hivyo kumuathiri mtoto kimwili, kisaikolojia, kitabia au kwa mchanganyiko wa maeneo yote matatu.
- Madhara yanatofautiana kutegemeana na:
  - mazingira ya unyanyasaji au kutojaliwa
  - wasifu wa mtoto binafsi
  - mazingira ya mtoto.

Mambo Yanayochangia Athari Za Unyanyasaji Na Kutojaliwa Mtoto(Inaendelea)

- Tafiti pia zimeanza kutafuta sababu kwanini katika mazingira yanayofanana watoto wengine hupata athari za muda mrefu ya unyanyaswaji na kutojaliwa wakati wengine hufikia utu uzima wakiwa na matatizo machache.
- Uwezo wa kukabiliana na hali na hatimae kuendelea kustawi, baada ya kupata uzoefu mbaya(hasi) Mara nyingine hujulikana kama “ukimya”.

Mambo Yanayochangia Athari Za Unyanyasaji Na Kutojaliwa Mtoto...

Si watoto wote walionyanyaswa na kutojaliwa watapata athari za muda mrefu. Matokeo ya mtu mmojammoja yanatofautiana sana na yanachangiwa na mchanganyiko wa sababu zikiwa ni pamoja na:

- Umri wa mtoto na hatua ya maendeleo ya makuzi wakati unyanyasaji na kutojaliwaa kumetokea.
- Aina ya unyanyasaji (kimwili, kutojaliwa, unyanyasaji wa kingono n.k.)
- Amenyanyaswa mara ngapi, Muda na athari za manyanyaso
- Mahusiano baina ya mhanga na mnyanyasaji

Chanzo:(English et al. 2005, Chalk, Gibbons, & Scarupa, 2002)

Mambo Yanayochangia Athari Za Unyanyasaji Na Kutojaliwa Mtoto...

- Watafiti pia wameanza kuchunguza sababu zinazofanya watoto wengine wapate madhara ya muda mrefu ya unyanyaswaji na kutojaliwa wakati watoto wengine hawapati athari zozote pamoja na kuwa wote wako katika mazingira yanayofanana.
- Uwezo wa kukabiliana na hali, na kustawi, kufuatia kupitia hali mbaya mara nyingine hujulikana kama “kukubaliana na hali kulingana na mazingira”

Child Welfare Information Gateway. (2008). Long-term consequences of child abuse and neglect. Washington, DC: USDHHS

Mambo Yanayochangia Athari Za Unyanyasaji Na Kutojaliwa Mtoto...

- ***Sababu kadhaa za ulinzi na za kuendeleza zinaweza kuchangia kuwa na uwezo wa kukabiliana na hali kulingana namazingira kwa mtoto anaye pitia unyanyasaji au kutojaliwa. Sababu hizi ni pamoja na:***
  - Sifa za mtu binafsi, msimamo wa kutegemea mazuri, kujiamini, ufahamu,ubunifu, hali ya mtu, na uhuru,
  - Vilevile kukubalika kwake na wana rika na mwitikio chanya wa mtu binafsi kwa waalimu, mnasihi, na mfano wa kuigwa.
  - Sababu nyinginezo ni pamoja na mazingira ya kijamii ya mtoto na uwezo wa familia katika kumpatia huduma za kijamii.
  - Usalama wa jamii, ikiwemo uimara wa majirani na upatikanaji wa shule salama pamoja na huduma za afya zakutosha, ni sababu zingine za ulinzi na maendeleo. (Fraser & Terzian, 2005).

Sababu Zinazofanya Mtoto Kuwa Katika Hatari Ya Kunyanyaswa Au Kutojaliwa

- Tofauti katika athari za muda mrefu kwa mtoto mmoja mmoja aliyenyanyaswa /kutojaliwa zimepelekea kufanyika utafiti unaoangalia sababu zinazomfanya mtoto awe katika hatari na mambo yanayoweza kumlinda au kumfanya awe na ukimya vitu vinavyomuepusha kunyanyaswa au kutengwa. Sababu hizi ni pamoja na zile za mtoto, mzazi, au mlezi na mazingira.

Sababu za Hatari na Ulinzi Kwa Unyanyasaji na Kutojaliwa Mtoto

Sababa Za Hatari Na Ulinzi

- Ni upi wito wa mpango wa wasaidizi ustawi?

Sababu Za Hatari Na Ulinzi

- Watoto kwanza, kuwalinda watoto, kuimarisha familia.
- Waweke watoto kwanza kwa kuwalinda watoto na kuimarisha familia.

Sababu Za Hatari Na Ulinzi

- Ni muhimu haswa kuweka wito wetu katika matendo wakati watoto wanaponyanyaswa au wanapokuwa katika hatari ya kunyanyaswa.
- Tayari tumeshazingatia kuwa unyanyasaji wa watoto unaendelea na tunahitaji kuingilia kati.
- Ili kuwalinda watoto na kuimarisha familia ni muhimu pia kuweza:
- Kutambua dalili kuwa mtoto yuko katika hatari ya kunyanyaswa na
- kuzisaidia familia kutoa malezi mazuri kwa watoto wao.

Sababu Za Hatari Na Ulinzi

- Hivyo tutatumia muda wetu uliobaki leo pamoja :
- Kutambua njia mbalimbali ambazo watoto, wazazi, na mazingira yao yanawaweka watoto katika hatari ya kunyanyaswa
- kutambua njia zinazoonekana kusaidia kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji na kuwezesha familia na mtoto kuhimili
- kutengeneza mipango ya kuingilia kati kupunguza hatari na kuwezesha sababu za ulinzi na kuhimili kwa mtoto na familia.

Sababu Zinazomfanya Mtoto Awe Katika Hatari Ya Kunyanyaswa Na Kutojaliwa.

- Tofauti iliyopo kwa madhara ya muda mrefu ya unyanyasaji na kutojaliwa kwa mtoto mmoja mmoja kumepelekea kutafiti kuhusu mambo yanayomuweka mtoto katika hatari, sababu za ulinzi na sababu zinazomfanya aweze kukabiliana na hali kulingana na mazingira ambazo zinamkinga dhidi ya unyanyasaji na kutojaliwa.
- Sababu hizi ni pamoja na:
- Sababu za mtoto mwenyewe(afya,tabia, hadhi ya mtu, Tabia na mtazamo wa Mzazi au mlezi.
  - matukio na au mazingira ya kijamii

Zoezi Kuhusu Sababu Za Hatari

- Fanya kazi na wenzako wawili kufanya kundi dogo la watu 3
- Jaribu kuorodhesha
  - Hatari moja inayohusiana na mtoto
  - Hatari moja inayohusiana na mzazi au mlezi
  - Hatari moja inayohusiana na jamii

Zoezi Kuhusu Sababu Za Hatari

- Je kila kundi lime tambua hatari gani zinazohusiana na mtoto?
- Baada ya kuorodhesha rejea maelezo yaliyoandaliwa(angalia mwongozo) kuongezea au kujadili

Sababu Za Hatari Kwa Mtoto

- Kuzaliwa kabla ya siku zake au kasoro za kimaumbile
- Kupata sumu wakati angali tumboni kwa mama yake
- Magonjwa sugu au ya hatari
- Tabia ya mtu-Vigumu kuwa mpole au kukasirika
- Mtindio wa ubongo /Uwezo mdogo wa kiakili
- Mshtuko wa maono wakati wa utoto
- Tabia mbaya za kijamii katika makundi rika

Zoezi La Sababu Za Hatari

- Je kila kikundi kimetambua hatari gani zinazohusiana na mzazi au mlezi?
- Baada ya kuorodhesha rejea maelezo yanayofuata kuongezea au kujadili

Sabau Za Hatari Zitokanazo Na Mzazi/Familia

- Ukaribu usio salama
- ***Wazazi:*** Ukaribu na wazazi usio salama
- Ulezi pweke (na kukosa msaada)
- Malezi ya kikatili na yasio sahihi
- Familia kutokuwa na mpangilio: ufuatiliaji mdogo wa malezi
- Kujitenga katika mambo ya kijamii, kukosa msaada
- Ugomvi wa majumbani

Sababu Za Hatari Zitokanazo Na Mlezi/Familia...

- ugomvi wa wazazi wa hali ya juu
- Kutengana/Kuachana, hususan kuachana kwa kugombana
- Tatizo la kisaikolojia kwa wazazi
- Matumizi ya madawa kwa wazazi
- Kuugua kwa wazazi
- Kufiwa na mzazi au mwana familia
- Kupelekwa kwenye malezi ya kambo

Zoezi La Sababu Za Hatari

- Je kila kikundi kimetambua hatari gani zinazohusiana na jamii au mazingira?
- Baada ya kuorodhesha rejea maelezo yanayofuata kuongezea au kujadili

Sababu Za Hatari Kijamii/Kimazingira

- Umasikini
- Kukosekana kwa huduma za kitibabu, Bima ya afya na huduma za jamii
- Mlezi kutokuwa na ajira
- Kutokuwa na makazi
- Malezi yasiyotosheleza kwa mtoto
- Ubaguzi unaotokana na madaraja au asili ya mtu n.k.
- Shule duni

Sababu Za Hatari Kijamii/Kimazingira

- Kuhamahama mara kwa mara makazi na shule
- Kuwa katika mazingira yenye sumu
- Majirani walio hatarishi
- Vurugu/magomvi katika jamii
- Kuwa katika mazingira yenye vurugu za vyombo vya habari

Sababu Za Ulinzi

- Fikiria kuhusu uzoefu wako wakufanya kazi na watoto pamoja na familia, je umegundua sifa zozote zinazoshabihiana kwa mtoto, mzazi au mazingira ikiwa mtoto ana malezi mazuri? Bungua bongo
- Tunaziita sababu za ulinzi
- Tunaweza pia kuzigawa katika makundi:
- kwa mtoto
- Kwa Mzazi/mlezi
- Kwa Jamii/mazingira

Zoezi Kuhusu Sababu Za Ulinzi

- Fanya kazi na wenzako wawili kufanya kundi dogo la watu 3
- Jaribu kuorodhesha
  - Sababu moja ya ulinzi inayohusiana na mtoto
  - sababu moja ya ulinzi inayohusiana na mzazi au mlezi
  - Sababu moja ya ulinzi inayohusiana na jamii

Zoezi La Sababu Za Ulinzi

- Je kila kikundi kimetambua sababugani za ulinzi zinazohusiana na mtoto?
- Baada ya kuorodhesha rejea maelezo yanayofuata kuongezea au kujadili

Sababu Za Ulinzi Kwa Mtoto

- Afya bora
- Sababu za hali ya mtu binafsi: (easy temperament) Kuwa chanya kujiweka kwenye nafasi; Anaechukuliana na hali vizuri, kujiamini kwa hali ya juu, stadi nzuri za kijamii, uwezo wa ndani wa kujitawala, anaweza kuweka usawa kati ya kutafuta msaada na kujitawala mwenyewe
- Ana akili juu ya wastani
- Historia ya maendeleo ya kutosha
- Shughuli/Masuala anayo yapendelea
- Mahusiano mazuri ya wanarika

Davies, D. (2004). Child Development: A Practitioner's Guide. New York: Guilford pp. 106-108

Zoezi La Sababu Za Ulinzi

- Je kila kikundi kimetambua sababu gani za ulinzi zinazohusiana na mzazi au mlezi?
- Baada ya kuorodhesha rejea maelezo yanayofuata kuongezea au kujadili

Sababu Ya Ulinzi Kwa Walezi/Familia

- Ukaribu ulio salama: chanya na mahusiano mazuri kati ya mzazi na mtoto
- ***Mzazi:*** Humsaidia mtoto wakati anapokuwa na msongo
- Muundo na sheria za nyumbani: jinsi wazazi wanavyomfuatilia mtoto
- Msaada/ kujihusisha na wanandugu wengine, ikiwemo msaada wa malezi
- Mahusiano mazuri kati ya wazazi
- Mtindo wa malezi thabiti ya wazazi na stadi nzuri za kukabiliana na hali
- Matarajio ya familia kuhusu tabia za kijamii
- Wazazi kuwa na kiwango cha juu cha elimu

Zoezi La Sababu Za Ulinzi

- Je kila kikundi kimetambua sababu gani za ulinzi zinazohusiana na mazingira au jamii?
- Baada ya kuorodhesha rejea maelezo yanayofuata kuongezea au kujadili

Sababu Za Ulinzi Kijamii Na Kimazingira

- Rasilimali za kutosha kwa ajili ya mahitaji ya msingi
- Hali ya kati au hali ya kiuchumi ya juu
- Upatikanaji wa huduma za afya na huduma za kijamii
- Mzazi kuwa na ajira yenye mwendelezo
- Kuwa na nyumba inayofaa
- Kujihusisha kwa familia katika masuala ya kidini na imani
- Shule nzuri
- Watu wazima nje ya familia hutoa msaada kwa kuwa mfano wa kuigwa/kufundisha watoto

Kutengeneza Mipango Ya Afua Kusaidia Kwa Kutumia Sababu Za Hatari Na Ulinzi.

- ***Mikakati ya kupunguza sababu za hatari na kuendeleza sababu za ulinzi au uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira, kumeonekana kuwa na ufanisi zaidi iwapo:***
- Ina anza mapema na kuendelea kwa miaka mingi
- inapojumuisha kazi nyingi na zinahusisha kukutana mara kwa mara
- inashughulika moja kwa moja na mtoto na mzazi
- Inapo jumuisha karibu kila kitu: ikiwemo afya, elimu, mahitaji
- halisi ya familia
- inashughulika na Hatari halisi/ Mahusiano imara
- Kuendelea kushughulikia na kusaidia

Upimaji Ya Sababu Za Hatari Na Ulinzi

Visababishi vya hatari	Vizuizi vya hatari
Mtoto	
Familia	
Kijamii/mazingira	

Upimaji Ya Sababu Za Hatari Na Ulinzi: Zoezi La Kundi Kubwa

Ili kufanya mazoezi ya kutumia sababu za hatari na ulinzi kuelewa mahitaji na uwezo wa mtoto na familia, tufikirie kuhusu Mwakaila, familia yake na jamii kisha jinu maswali yafuatayo:

- Ni hatari gani unazoweza kuzitambua kwa mtoto, familia na mazingira?
- Ni sababu gani za ulinzi unzoweza kuzitambua kwa mtoto, familia na mazingira?

Tutarekodi majibu ya maswali yetu kwenye dodoso la upimaji ya sababu za hatari na ulinzi.

Tumia Sababu Za Hatari Na Ulinzi Kutengeneza Mpango Wa Afua.

- ***Aina ya mipango ya kushughulikia unyanyasaji wa mtoto na kutojaliwa:***
  - Mipango inayoweza kupunguza hatari
  - Mipango inayoweza kuendeleza uwezo wa kukabiliana na hali kulingana na mazingira au sababu za ulinzi.
  - Angalizo: mipango ya aina zote inahitajika kupangiliwa katika ngazi tatu tofauti. (i) mtoto (ii) mlezi na (iii) mazingira ya kijamii

Upimaji Ya Sababu Za Hatari Na Ulinzi

- ***Unapofanya uchambuzi wa sababu za hatari na ulinzi ili kutengeneza mpango:***
  - Tambua sababu za hatari ukianzia na sababu ya hatari zaidi
  - Tambua sababu zozote za ulinzi zinazoweza kuimarishwa ili kupunguza hatari kwa kila sababu ya hatari.
  - Tengeneza mpango wa utekelezaji kumlinda mtoto kwa kushughulikia hatari mojamoja iliyotambuliwa.

Mpango Wa Kushughulikia Sababu Za Hatari Na Ulinzi: Zoezi La Kundi Kubwa

- Fikiria kuhusu sababu za hatari na ulinzi ulizozitambua kwa Mwakaila,familia yake na jamii.
- Tufanye kwa vitendo kwa kutengeneza mpango wa afua kwa Mwakaila na tuweke kumbukumbu kwenye dodoso linalofuata.

Kutengeneza Mpango Wa Afua

(Anza na hatari ya juu zaidi)

	Sababu ya hatari	Sababu ya ulinzi	Mpango wa afua
mtoto			
Mzazi/mlezi			
Jamii/mazingira			

Zoezi La Vikundi Vidogo

- Gawa vikundi vinne
- Chagua mwakilishi mmoja katika kikundi atakaye toa mrejesho wa mliyojifunza katika kundi kubwa
- Tambua mtoto na mwanafamilia ambayo mmoja wa wanakikundi ana fanya kazi nao kisha mwanakikundi aelezee hali halisi ya familia katika kundi kubwa.
- Mkiwa katika vikundi muainishe sababu za hatari kwa mtoto, familia na jamii kisha mziandike.

Zoezi La Vikundi Vidogo

- Mkiwa katika kikundi Muainishe sababu za ulinzi kwa mtoto, familia na jamii kisha muandike
- changanua sababu za ulinzi na hatari mkianza na zile zenye hatari zaidi kisha muandae mpango wa kushughulikia ili kupunguza sababu za hatari na kuendeleza sababu za ulinzi
- Weka kumbukumbu za taarifa kuhusu mpango wa kushughulikia kwenye dodoso mlilopewa.
- Jadili kuhusu uzoefu na muainishe mambo mliyojifunza kutokana na mchakato huu unaoweza kuutumia kwenye utendaji wako wa kilasiku

Mrejesho Toka Katika Vikundi

Muhtasari Na Mrejesho Wa Siku